
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI**

# TAARIFA YA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2023 NA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2024/25














**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI, MHESHIMIWA PROF. KITILA ALEXANDER MKUMBO (Mb.).**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI**

# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI, MHESHIMIWA PROF. KITILA ALEXANDER MKUMBO (MB.) AKIWASILISHA BUNGENI

# TAARIFA YA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2023 NA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2024/25

**DODOMA**

**Juni 2024**

# A.

## Utangulizi

1 ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25. Pamoja na Hotuba hii, ninawasilisha vitabu vya Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25. Taarifa zilizopo katika vitabu hivi ndiyo msingi wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/25, ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha ataiwasilisha katika Bunge lako Tukufu leo alasiri.

2 ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote ninamshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kutuwezesha kuendelea kushiriki Mkutano wa 15 wa Bunge hili la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tukiwa na afya njema, amani na utulivu. Aidha, ninakushukuru wewe ***Mheshimiwa Spika,*** Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuendesha majadiliano ya Bunge hili la Bajeti kwa umahiri mkubwa tangu siku Mheshimiwa Waziri Mkuu alipowasilisha hotuba yake ya Bajeti, na baadaye hotuba za bajeti za mawaziri wenzangu hadi leo hii tunapoelekea kuhitimisha kwa hotuba yangu hii na baadaye alasiri Hotuba ya Bajeti ya Serikali itakayosomwa na Waziri wa Fedha.

3 ***Mheshimiwa Spika,*** Ninapenda kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jinsi anavyoendelea kuliongoza Taifa letu kwa weledi, umahiri na utulivu mkubwa. Katika kipindi chake cha miaka mitatu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameonesha weledi na kuthibitisha uadilifu na uzalendo wa hali ya juu kwa nchi yake. Zaidi ya yote, amethibitisha kuwa kiongozi muungwana na mpenda haki. Kupitia falsafa yake ya 4R, amejenga maridhiano mapana ya kijamii na kisiasa na kuweka mazingira sawia ya kufanya siasa kwa vyama vyote nchini (R1 =Reconciliation); ametoa uhuru wa kutosha wa kutoa maoni bila woga wala vitisho huku akionesha ustahimilivu wa hali ya juu (R2=Resilience). Kiongozi wetu ameleta mageuzi makubwa katika kuweka mazingira bora ya biashara na uwekezaji (R3 = Reform). Ameimarisha sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na madini na kuwapa matumaini mapya mamilioni ya wakulima, wafugaji, wavuvi na wachimbaji wadogo wa madini. Hakika anaijenga upya nchi yetu (R4 =Rebuilding) na kupitia uongozi wake, Serikali na nchi yetu ipo salama.

4 ***Mheshimiwa Spika,*** ninawashukuru pia Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko(Mb.), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa jinsi wanavyomsaidia Mheshimiwa Rais katika kusimamia programu na miradi mbalimbali ya maendeleo katika nchi yetu. Aidha, ninamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa uongozi wake mahiri katika kuiongoza Zanzibar kuelekea maendeleo endelevu na makubwa zaidi kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050.

5 ***Mheshimiwa Spika,*** ninawashukuru Dkt. Tausi Mbaga Kida, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, Ndugu Lawrence Nyasebwa Mafuru, Katibu Mtendaji Tume ya Mipango, na watumishi wote wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Tume ya Mipango kwa ushirikiano wao katika kuandaa hotuba hii na vitabu vyake.

6 ***Mheshimiwa Spika,*** ninampongeza Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mbunge wa Maswa Mashariki, kwa heshima aliyopata ya kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Ninamfahamu Mheshimiwa Nyongo katika kipindi cha uhai wa Bunge hili la 12, nikiwa nimefanya naye kazi kwa karibu kwa iliyokuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, ambapo yeye alikuwa mwenyekiti wake. Ni mtu makini, mtulivu, msikivu, mpana wa fikra na mwenye kuthamini sana mawazo na maoni ya wenzake. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutuletea kiongozi huyu tusaidiane naye katika kuongoza ofisi yake hii muhimu sana katika kupanga na kusimamia mipango ya maendeleo ya nchi yetu, pamoja na kuhakikisha kuwa nchi yetu inaendelea kuwa eneo salama na la kuvutia wawekezaji.

7 ***Mheshimiwa Spika,*** maeneo mengi ya nchi yetu yamepata mvua nyingi zilizo juu ya wastani, hali iliyosababisha mafuriko katika maeneo mbalimbali. Mafuriko haya yamesababisha vifo kwa baadhi ya watanzania, uharibifu mkubwa wa mazao ya wakulima, mali na miundombinu, hususan barabara na madaraja. Mafuriko hayo yameathiri utelekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuongeza gharama za ukarabati wa miundombinu iliyoharibika. Kwa msingi huo, baadhi ya miradi ya maendeleo inatarajiwa kuchelewa kuanza na kukamilika. Hata hivyo, niwahakikishie watanzania kuwa Serikali imejipanga vyema katika kuhakikisha kuwa miundombinu iliyoharibiwa inakarabatiwa na kurudi katika hali ya kawaida.

8 ***Mheshimiwa Spika,*** Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25 zimeandaliwa kwa kuzingatia dhana ya ushirikishwaji mpana wa wadau katika hatua za maandalizi na ufanyaji maamuzi katika ngazi mbalimbali Serikalini. Nitumie nafasi hii kuwashukuru wadau wote walioshiriki katika kuandaa Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25. Kwa njia ya pekee, ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Oran Manase Njeza (Mbunge wa Mbeya Vijijini), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti na wajumbe wote wa Kamati kwa ushauri na maoni yao wakati wa uandaaji wa taarifa nilizowasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu.

9 ***Mheshimiwa Spika,*** Hotuba yangu ipo katika sehemu kuu Sita. Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi. Sehemu ya Pili ni Mwenendo wa Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2023. Sehemu ya Tatu ni Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24. Sehemu ya nne ni Malengo na Vipaumbele katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25. Sehemu ya tano ni Hitimisho.

# B.

# Mwenendo na Mwelekeo wa Hali ya Uchumi

## Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Dunia

10 ***Mheshimiwa Spika,*** Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha Kimataifa (IMF) ya mwezi Aprili 2024, matarajio ya msingi (baseline forecast) ni kuwa uchumi wa dunia utaendelea kukua kwa asilimia 3.2 mwaka 2024 na 2025, kwa kasi sawa na mwaka 2023. Matarajio haya ya ukuaji wa uchumi wa dunia kwa asilimia 3.2 ni wa kiwango cha chini ukilinganisha na wastani wa kihistoria wa miongo miwili iliyopita (2000-2019) wa asilimia 3.8.

11 ***Mheshimiwa Spika,*** Kiwango cha ukuaji wa uchumi wa nchi zilizoendelea kilipungua na kufikia asilimia 1.6 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 2.6 mwaka 2022. Ongezeko dogo la kasi ya ukuaji wa uchumi wa mataifa

yaliyoendelea la asilimia 1.6 mwaka 2023 hadi matarajio ya asilimia 1.7 mwaka 2024 na asilimia 1.8 mwaka 2025 linachangiwa na madhara ya vita inayoendelea kati ya Urusi na Ukraine ambayo kwa kiasi kikubwa imeyumbisha siyo tu uchumi wa nchi za Ulaya bali hata uchumi wa dunia nzima kutokana na kuongezeka kwa gharama za maisha kulikosababishwa na mfumuko wa bei za nishati barani Ulaya na bei za vyakula katika soko la dunia.

12 ***Mheshimiwa Spika,*** Ukuaji wa uchumi kwa ukanda wa nchi zinazoibukia (emerging economies) na zinazoendelea kiuchumi (developing economies) uliendelea kustahimili madhara yaliyotokana na vita kati ya Urusi na Ukraine ambayo yaliathiri uchumi wa nchi nyingi duniani. Kiwango cha ukuaji wa uchumi wa nchi zilizopo katika kundi hili uliimarika na kufikia wastani wa asilimia 4.3 mwaka 2023 ukilinganisha na asilimia 4.1 mwaka 2022, na matarajio ni kuendelea na ukuaji wa asilimia 4.2 mwaka 2024 na mwaka 2025.

13 ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Taarifa ya IMF ya Aprili 2024 inaonesha kuwa kiwango cha ukuaji wa ulikuwa wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2023 ikilinganishwa na 4.9 mwaka 2022. Aidha, ukuaji wa uchumi kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ulikuwa wa wastani wa asilimia 4.4 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.2 mwaka 2022.

## Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Taifa

14 ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2023, Pato halisi la Taifa lilifikia shilingi trilioni 148.3 kutoka shilingi trilioni 141.2 mwaka 2022, sawa na ukuaji wa asilimia 5.1 ikilinganishwa na asimilia 4.7 mwaka 2022. Ukuaji huo ulichangiwa na jitihada mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali ikiwemo: mikakati ya kukabiliana na athari za vita kati ya Ukraine na Urusi pamoja na uwekezaji wa kimkakati katika miundombinu ya nishati, maji, afya, elimu na usafirishaji; kuongezeka kwa uzalishaji wa madini, hususan dhahabu na makaa ya mawe; na kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi iliyochachua shughuli za kiuchumi.

15 ***Mheshimiwa Spika,*** Mfumuko wa bei nchini ulifikia asilimia 3.1 katika kipindi kilichoishia mwezi Aprili 2024 ikilinganishwa na asilimia 4.3 katika kipindi kama hicho Mwaka 2023. Aidha, mfumuko wa bei ulifikia wastani wa asilimia 3.8 Mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.3 Mwaka 2022. Kiwango hiki ni cha chini ikilinganishwa na nchi wanachama wa EAC na kipo ndani ya malengo ya kati ya asilimia 3.0 hadi 7.0 na vigezo vya mtangamano

wa kiuchumi kikanda (EAC na SADC). Kupungua kwa mfumuko wa bei pamoja na mambo mengine kumetokana na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti na kuanza kuimarika kwa upatikanaji wa mazao ya chakula katika masoko ya ndani na ya nchi jirani.

16 ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 urari wa malipo yote ya nje uliendelea kuimarika na kuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,616.4 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 3,977.8 kwa kipindi kama hicho mwaka 2023. Aidha, thamani ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 6,016.2, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 5,629.2 kwa kipindi kama hicho mwaka 2022. Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na mauzo ya dhahabu na bidhaa asilia, hususan tumbaku, korosho na kahawa, pamoja na mauzo ya mazao ya mboga na maua.

17 ***Mheshimiwa Spika,*** Akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa ya kuridhisha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi. Hadi kufikia Machi 2024, kiwango cha akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani milioni 5,327.1 ukilinganisha na dola za Marekani milioni 5,012.5 katika kipindi kama hicho Mwaka 2022. Kiasi hicho kinatosheleza malipo ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha miezi 4.4, zaidi ya lengo la nchi la kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayokidhi uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi isiyopungua 4.0.

18 ***Mheshimiwa Spika,*** mikopo katika sekta binafsi imeendelea kuwa imara hadi kufikia ukuaji wa shillingi billioni 33,746.5, sawa na asilimia 17.6, kutoka ukuaji wa shillingi billioni 28,702.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Sekta zilizochangia ukuaji huo ni: Sekta ya Kilimo kwa asilimia 60.6; viwanda na biashara kwa asilimia 29.1; sekta ya uchimbaji wa madini asilimia 18.1; na mikopo kwa shughuli binafsi asilimia 16.7. Ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi, hususan katika sekta za kilimo, viwanda na uzalishaji, na uchimbaji madini, linaashiria uimarishaji wa mazingira ya biashara na ukuaji wa shughuli za kiuchumi. Hatua za kisera zilizolenga kupunguza viwango vya riba na kuongeza bajeti katika sekta muhimu kama kilimo zimeonekana kuwa na matokeo chanya katika kuchochea ukuaji huu.

19 ***Mheshimiwa Spika,*** Hadi kufikia Machi 2024, deni la Serikali lilikuwa shilingi bilioni 91,708.3. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 30,753.8 na deni la nje lilikuwa shilingi bilioni 60,954.5. Aidha, ongezeko la deni lilitokana na Serikali kuendelea kupokea fedha za mikopo ya zamani na mipya kutoka vyanzo mbalimbali kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo, ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege, umeme na maji. Vile vile, ongezeko la deni lilichangiwa na kupanda

kwa viwango vya kubadilisha fedha pamoja na kuongezeka kwa riba kwenye mikopo ya nje ambayo riba zake hutegemea mabadiliko ya hali ya soko.

20 ***Mheshimiwa Spika,*** Kwa mujibu wa Taarifa ya Dunia ya Maendeleo ya Watu ya Mwaka 2023, Tanzania imeendelea kupiga hatua kwa kuzingatia Fahirisi ya Maendeleo ya Watu - HDI ambapo ilifikia 0.532 mwaka 2022 ikilinganishwa na 0.529 mwaka 2021. Kipimo hiki kinatafsiriwa kuwa kadiri tarakimu inavyokaribia moja (1), inaashiria kuimarika kwa maendeleo ya watu. Katika kuhakikisha, Tanzania inapiga hatua katika kushika nafasi bora zaidi kidunia, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi itaendelea kuweka mikakati ya kuimarisha utoaji wa huduma za msingi ikiwemo afya, elimu, maji na kuboresha hali ya Maisha.

## Tathmini ya muda mrefu ya hali ya uchumi wa Taifa

21 ***Mheshimiwa Spika,*** Tathmini ya muda mrefu ya uchumi wa Tanzania inaonesha masuala makubwa matatu. Mosi, uchumi umekuwa stahimilivu na kukua katika hali endelevu licha ya changamoto zilizoyumbisha uchumi wa dunia katika vipindi mbalimbali, ikiwemo mabadiliko ya tabia nchi, ugonjwa wa UVIKO – 19, na vita mbalimbali. Pili, kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi iliongezeka kutoka dola za Marekani milioni 975 mwaka 2000 hadi kufikia dola za Kimarekani bilioni 5.63 mwaka 2020, na kufikia dola za Marekani bilioni 8.20 mwaka 2023. Hali hii ilisababisha kuongezeka kwa uwiano kati ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi kutoka asilimia 9.6 mwaka 2000 hadi asilimia 20.9 mwaka 2023. Tatu, aina ya bidhaa za Tanzania zinazouzwa nje ya nchi zimebadilika katika kipindi cha miongo miwili iliyopita. Kwa mfano, katika miaka ya 2000 asilimia ya 57 ya mauzo ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi ilihusisha mazao ya kilimo katika masoko ya Ulaya, Marekani, na Afrika. Hata hivyo, miaka 20 baadaye, mauzo ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi yametawaliwa zaidi na madini na bidhaa nyingi zinauzwa katika masoko ya Asia na nchi za Afrika. Kwa mfano, asilimia 49 ya bidhaa zilizouzwa nje ya nchi mwaka 2023 ilikuwa ni madini, ikifuatiwa na bidhaa za viwandani (17%) na mazao ya kilimo (12%).

22 ***Mheshimiwa Spika,*** Kwa mujibu wa taarifa ya Hali ya Uchumi wa Tanzania ya Benki ya Dunia ya Septemba 2023, uchumi wa Tanzania umeendelea kuimarika na kuhimili vyema athari za UVIKO - 19 na changamoto zingine za dunia zilizojitokeza katika miaka mitatu iliyopita kutokana na sababu kubwa tatu. Mosi, utekelezaji wa mageuzi makubwa yaliyolenga katika kuchochea na kuimarisha ushindani katika uchumi, sambamba na eneo la kwanza la kipaumbele katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka

Mitano 2021/22 – 2025/26 -"Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi". Pili, kuendelea kuboresha na kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini. Tatu, kuendelea kuaminiwa na taasisi za fedha duniani, pamoja na wadau wetu wa maendeleo. Hii ilithibitishwa pia na taarifa ya tathmini iliyotolewa na Taasisi ya Moody's ya Machi 2024 ambayo ilibadili kipimo (rating) cha Tanzania kutoka imara (stable) kwenda chanya (positive). Katika taarifa yao, taasisi hii walieleza kuwa uchumi wa Tanzania umeendelea kuimarika katikati ya changamoto nyingi za dunia ukionesha ustahimilivu mkubwa. Sababu zilizotolewa na Taasisi ya Moody's ni pamoja na Tanzania kuwa na msingi mzuri wa uchumi mchanganyiko (diversified economy), kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa nje ya nchi, ustahimilivu wa deni, sera imara za kifedha, pamoja na kuendelea kuimarika na kuboreka kwa mazingira ya biashara na uwekezaji.

23 ***Mheshimiwa Spika,*** Pamoja na mwelekeo mzuri wa ukuaji wa uchumi wa Tanzania katika kipindi cha miongo miwili iliyopita mambo matano ni bayana kuhusu uchumi wa Tanzania. Mosi, ukuaji wa uchumi umekuwa ukihusisha sekta chache na ambazo haziajiri watu wengi kutoka kaya maskini. Sekta zilizoongoza kwa ukuaji kwa mwaka 2023 ni pamoja na Sanaa (17.7%), fedha na bima (12.2%), madini (11.3%) na malazi na chakula (8.3%). Sekta ambazo zilitarajiwa kuajiri watu wengi zilikua kwa kasi ndogo. Sekta hizi ni pamoja na kilimo (4.2%), viwanda (4.3%) na biashara (4.2%). Matokeo ya hali hii ni kwamba ukuaji wa uchumi umekuwa hauendani na kasi ya kupunguza umaskini kwa kiwango cha kuridhisha. Pili, ukuaji wa uchumi nchini umekuwa ukitegemea uwekezaji wa umma katika miundombinu na sekta binafsi haijaonekana kuchukua nafasi yake kikamilifu katika kuchochea ukuaji wa uchumi kama ilivyotarajiwa. Uwekezaji kupitia sekta binafsi ndio unaotarajiwa kuchochea ajira na uzalishaji. Tatu, mauzo ya bidhaa nje ya nchi yameendelea kutegemea bidhaa ambazo hazijaongezwa thamani. Kwa mfano, wakati uzalishaji viwandani ulitarajiwa kuchangia asilimia 24 ya mauzo ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi ifikapo mwaka 2025 mchango wa sekta hii kwa wastani wa miaka mitano (2019-2023) ulikuwa asilimia 17.1 pekee (ukilinganisha na asilimia 16.9 mwaka 2019/20). Hii inamaanisha kuwa mauzo haya hayajachangia vya kutosha katika kuzalisha ajira. Nne, nchi yetu bado inanunua zaidi kutoka nje kuliko kiwango tunachouza. Hivyo, bado tuna urari mkubwa katika biashara. Kwa mfano, thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi kwa mwaka 2023 ilikuwa Dola za Kimarekani bilioni 8.2 ukilinganisha na thamani ya manunuzi ya bidhaa ambazo Tanzania iliagiza kutoka nje ya nchi ya Dola za Kimarekani bilioni 13.7. Hii ndiyo kusema nchi yetu bado inatumia fedha nyingi za kigeni kuagiza bidhaa ambazo zingeweza kuzalishwa nchini. Tano, uchumi umekuwa ukikua kwa kasi zaidi katika maeneo ya mijini kuliko vijijini.

24 ***Mheshimiwa Spika,*** Ili kuhakikisha kuwa ukuaji wa uchumi unakuwa na athari chanya katika kuinua kiwango cha maisha ya watu na kupunguza umaskini, mipango ya muda mfupi na mrefu ijayo itajikita katika kuhakikisha kuwa ukuaji wa uchumi wetu unakuwa jumuishi, unapunguza umaskini, unazalisha ajira nyingi, unaleta ustawi na unachochea mauzo ya bidhaa zilizoongezwa thamani nje ya nchi.

## Mwelekeo wa hali ya uchumi wa taifa kwa Mwaka 2024

25 ***Mheshimiwa Spika,*** Malengo na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi Jumla ni kama ifuatavyo:

i. Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 5.4 mwaka 2024 kutoka ukuaji halisi wa asilimia 5.1 mwaka 2023;

ii. Kuendelea kudhibiti mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 - 5.0 katika muda wa kati;

iii. Mapato ya ndani kufikia asilimia 15.8 ya Pato la Taifa mwaka 2024/25 ikilinganishwa na matarajio ya asilimia 15.4 mwaka 2023/24;

iv. Mapato ya kodi kufikia asilimia 12.9 ya Pato la Taifa mwaka 2024/25 kutoka matarajio ya asilimia 12.6 mwaka 2023/24;

v. Kuwa na nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) isiyozidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa; na

vi. Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

26 ***Mheshimiwa Spika,*** maelezo ya kina ya taarifa ya Hali ya Uchumi yanapatikana katika Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa cha Mwaka 2023.

# C.

## Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo Wa Taifa Wa Mwaka 2023/24

27 ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2023/24 ni wa nne katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26), wenye kulenga kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu. Mpango huu wa miaka mitano una vipaumbele vitano vifuatavyo: Kuchochea uchumi shirikishi na shindani; Kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma; Kukuza uwekezaji na biashara; Kuchochea maendeleo ya watu; na Kuendeleza raslimali watu.

28 ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya programu na miradi 193 (ikiwemo miradi ya kielelezo 17) inatekelezwa katika kufikia malengo ya mpango wa miaka mitano kwa kuzingatia vipaumbele vilivyotajwa hapo juu.

29 ***Mheshimiwa Spika,*** katika katika kuchochea uchumi shindani na shirikishi, pamoja na mambo mengine, hatua zifuatazo zilichukuliwa:

i. Kuongeza uwezo wa uzalishaji katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi kwa kuongeza matumizi ya mbegu bora na mbolea, kuongeza eneo la umwagiliaji na kuanza ujenzi wa bandari ya uvuvi. Kwa mfano, matumizi ya mbolea yameongezeka kutoka tani 363,599 Mwaka 2020/21 hadi kufikia tani 580,628 mwaka 2022/23. Eneo la kilimo cha umwagiliaji limeongezeka kutoka Hekta 694,715 Mwaka 2019/20 hadi kufikia Hekta 727,280.6 Mwaka 2022/23.

ii. Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji, pamoja na miundombinu ya kidigitali kwa ajili ya kuchochea shughuli za kiuchumi na kijamii, ikiwemo:

   a. Ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha cha kimataifa (Standard Gauge Railway – SGR) ambapo utekelezaji wake ni kama ifuatavyo: Dar es Salaam -Makutupora (KM 300, 98.93%); Morogoro – Makutupora (KM 422, 96.61%); Makutupora – Tabora (KM 371, 14.22); Mwanza – Isaka (KM 341, 56.21%); Tabora – Isaka (KM 165, 5.38%); na Tabora – Kigoma (KM 506, 1.81%).

   b. Kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa uboreshaji Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) ambapo ndege mbili (2) aina ya Boeing 737-9 Max zimepokelewa na hivyo kufanya jumla ya ndege zinazomilikiwa na ATCL kufikia 16.

c. Kuendelea na uboreshaji wa Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Bandari Kavu ya Kwala (Ruvu)

d. Kuendelea kuboresha na kupanua mtandao wa barabara nchini ambapo hadi kufikia Aprili 2024 mtandao wa barabara uliongezeka na kufikia jumla ya kilometa 181,655.49.

e. Kuendelea na ujenzi wa Daraja la Kigongo-Busisi (Mwanza) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 88.

f. Kuendelea na upanuzi wa miundombinu ya digitali ili kupanua huduma za TEHAMA kwa wananchi

iii. Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kuzalisha na kusafirisha umeme, ikiwemo Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (MW 2,115) ambao umefikia asilimia 97.43.

iv. Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, na kuhamasisha wawekezaji kutoka nje na ndani ya nchi

30 ***Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ni pamoja na:

i. Kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo kutoka tani 30,569,893.52 mwaka 2020/21 hadi kufikia tani 36,409,694.83 Mwaka 2022/23. Uzalishaji wa mazao ya nafaka umeongezeka kutoka tani 9,046,377.10 mwaka 2020/21 hadi kufikia tani 11,420,327.06 mwaka 2022/23. Hali hii imeimarisha hali ya usalama wa chakula nchini ambapo hali ya utoshelevu wa chakula imefikia asilimia 124 mwaka 2022/2023 ikilinganishwa na lengo la kufikia asilimia 130 ifikapo mwaka 2025/2026.

ii. Kupungua kwa kiwango cha vifo vya mifugo kutoka asilimia 27 mwaka 2019/20 hadi asilimia 12 mwaka 2023/24; kuongezeka kwa uzalishaji wa nyama kutoka tani 702,000 mwaka 2019/20 hadi tani 803,264 mwaka 2023/24; kuongezeka kwa uzalishaji maziwa kutoka lita bilioni 3.01 mwaka 2019/20 hadi lita bilioni 3.97 mwaka 2023/24.

iii. kuongezeka kwa uzalishaji wa samaki kutoka tani 497,567.28 mwaka 2019/20 hadi tani 513,218.90 mwaka 2023/24

iv. Kuongezeka kwa uzalishaji wa umeme kutoka MW 1,872.1 Mwaka 2022/23 hadi kufikia MW 2,138 Machi 2024. Hii ni kutokana na kuanza uzalishaji umeme katika miradi ya Bwawa la Mwalimu Nyerere (MW 235), Kinyerezi I (MW 160) na Rusumo (MW 80). Aidha, jumla ya vijiji 11,837 (96.37% ya vijiji vyote Tanzania Bara) vimeunganishwa na umeme kufikia Desemba 2023.

v. Kuongezeka kwa watumiaji wa mtandao wa internet kutoka asilimia 43 mwaka 2019/20 hadi asilimia 58.1 mwaka 2023/24; kuongezeka kwa idadi ya watu waliofikiwa na masafa ya mawasiliano kutoka asilimia 45 mwaka 2019/20 hadi asilimia 86 (3G) na 79 (4G) mwaka 2023/24 na kuongezeka kwa maeneo yaliyofikiwa na masafa ya mawasiliano kufikia asilimia 70 (3G) na 63 (4G) mwaka 2023/24 ikilinganishwa na lengo la asilimia 80 ifikapo mwaka 2025/26; na kuongezeka kwa idadi ya kaya zinazotumia mfumo wa anwani za makazi na misimbo ya posta kutoka kaya 450,980 mwaka 2019/20 hadi kaya 11,126,234 mwaka 2023/24.

vi. Kuendelea kuimarika kwa mazingira ya biashara na uwekezaji, ambapo miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) iliongezeka kutoka miradi 207 kwa mwaka (Mwaka 2020) na kufikia miradi 526 kwa mwaka (Mwaka 2023), na kiwango cha mtaji kilichovutiwa kufika dola za Kimarekani bilioni 5.7 mwaka 2023 (kutoka dola bilioni 1.1 Mwaka 2020). Aidha, idadi ya ajira inayotokana na miradi ya uwekezaji imeongezeka kutoka 17,385 mwaka 2020 hadi kufikia 137,010 mwaka 2023.

vii. Kuongezeka kwa thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi kutoka dola za Kimarekani bilioni 5.63 mwaka 2020 hadi kufikia dola za Kimarekani bilioni 8.20 mwaka 2023. Aidha, katika kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani, kiwango cha mauzo ya bidhaa za viwandani (manufacturing goods) kiliongezeka kwa asilimia 20.8, kutoka dola za kimarekani milioni 1,109.3 mwaka 2021 na kufikia dola za kimarekani milioni 1,340.5 mwaka 2022 na baadaye kufikia dola za kimarekani milioni 1,401.2 mwaka 2023.

viii. Kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya msingi ilifikia asilimia 108.5 mwaka 2022, ikiwa ni zaidi ya lengo la kufikia asilimia 100 mwaka 2025/26. Aidha, kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi wa sekondari (Kidato cha I-IV) kimeongezeka kutoka asilimia 47.4 mwaka 2021 hadi asilimia 48.2 mwaka 2022, ikiwa ni zaidi ya lengo la kufikia asilimia 48 mwaka 2025/26.

ix. vifo vya watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano vimepungua kwa asilimia 36 kutoka vifo 67 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2015/2016 hadi kufikia vifo 43 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2022 .

x. Kupungua kwa vifo vitokanavyo na uzazi kutoka vifo 556 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2014/15 hadi vifo 104 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2022

xi. Katika sekta ya maji, utekelezaji wa miradi 630 yenye vituo 6,553 vya kuchotea maji vinavyonufaisha wananchi wapatao 4,393,274 kwenye vijiji 1,390 umekamilika, yenye uwezo wa kuhudumia asilimia 79.9 ya wananchi vijijini na asilimia 88 ya wananchi mijini. Kwa hatua hizi, kwa mujibu wa takwimu za sensa ya watu na makazi ya 2022, idadi ya kaya za vijijini nchini zinazopata maji safi na salama kutoka katika vyanzo vilivyoboreshwa kutoka zimeongezeka kutoka asilimia 36 mwaka 2019/20 hadi asilimia 56.1 mwaka 2022; na mijini kutoka asilimia 84 mwaka 2019/20 hadi kufikia asilimia 91.5 mwaka 2022.

xii. Kuongezeka kwa idadi ya watalii 1,527,230 mwaka 2019/20 hadi kufikia watalii 1,808,205 Mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 8.09 ya lengo la watalii 5,000,0000 ifikapo 2025/26. Aidha, mapato ya utalii yameongezeka kutoka dola za kimarekani bilioni 2.6 mwaka 2019/2020 kufikia dola za kimarekani bilioni 3.4 mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la asilimia 23 ikiwa ni jitihada za kufikia lengo la dola bilioni 6.0 mwaka 2025.

xiii. Kama sehemu ya mafanikio ya utekelezaji wa falsafa ya 4R, hususan Reform (Mageuzi), utawala wa sheria umeendelea kuimarika na demokrasia nchini imeendelea kupanuka kunakothibitishwa na kushamiri kwa uhuru wa kutoa maoni bila hofu ya kusumbuliwa.

# D.

# Malengo na Vipaumbele katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25

31 ***Mheshimiwa Spika,*** vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25 vimezingatia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26, Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 na Sera na Mikakati mbalimbali ya kisekta. Aidha, Mpango umezingatia mipango mingine ya kikanda na kimataifa zikiwemo Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) 2050; Dira ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) 2050; Agenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika; na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030.

32 ***Mheshimiwa Spika,*** Malengo ya jumla ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2024/2025 ni:

i. Kuendelea kulinda mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano iliyopita.

ii. Kuendelea na juhudi za kujitosheleza kwa mahitaji ya chakula nchini kwa kuendelea kuongeza matumizi ya mbolea, mbegu bora na kilimo cha umwagiliaji.

iii. Kuongeza uzalishaji na uuzaji wa bidhaa (pamoja na huduma) nje ya nchi kupitia sekta za kilimo, ufugaji, uvuvi, misitu na madini.

iv. Kuweka mkazo wa pekee katika kuongeza thamani katika mazao yanayozalishwa kupitia sekta za kilimo, ufugaji, uvuvi, misitu na madini

v. Kuendelea kuongeza, kuboresha na kuimarisha ubora wa huduma za jamii, ikiwa ni pamoja na elimu, afya, maji na umeme.

vi. Kuendelea kupanua na kuimarisha miundombinu ya usafiri wa barabara, reli, anga, na majini, na utunzaji endelevu wa mazingira.

vii. Kujielekeza kwenye kufungua fursa katika sekta za madini ya kimkakati (critical minerals), uvuvi wa bahari kuu (deep sea fishing), uchumi wa kijani (green economy) na uchumi wa kidigitali (digital economy). Maeneo haya matatu, ni maeneo yanayokamata kasi duniani kwa sasa, na ambayo kwa upande wetu hatujavuna ipasavyo.

viii. Kuendelea kuchukua hatua stahiki katika kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabia nchi, ikiwemo kuetekeleza mkakati wa miaka kumi wa matumizi ya nishati safi ya kupikia

ix. Kukamilisha maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

33 ***Mheshimiwa Spika,*** programu na miradi mahususi itakayotekelezwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25 imetajwa na kuanishwa katika Sura ya Tatu ya kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2024/25, na kama ambavyo ilianishwa kupitia Hotuba za Bajeti zilizowasilishwa hapa bungeni na mawaziri wa kisekta.

34 ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa ukuaji wa uchumi wetu unakuwa jumuishi, unapunguza umaskini, unazalisha ajira nyingi, unaleta ustawi na unachochea mauzo ya bidhaa zilizoongezwa thamani nje ya nchi, ninaomba kusisitiza masuala kumi (10) ambavyo Serikali ya Awamu ya Sita ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mwenyekiti wa CCM, itayapa msukumo wa kipekee katika mwaka ujao wa fedha.

i. Kuendelea kuwekeza katika kukuza uzalishaji katika sekta ya kilimo kwa kuhamasisha na kuwezesha matumizi ya mbegu bora, matumizi ya mbolea, kilimo cha umwagiliaji na matumizi ya zana za kisasa katika kilimo. Kama tunavyofahamu, uchumi wa viwanda tunaojaribu kuujenga malighafi zake nyingi zinategemea kilimo. Aidha, katika kipindi cha muda mfupi na muda wa kati, watanzania wengi wataendelea kuajiriwa na kujiajiri katika sekta ya kilimo. Hivyo, hatuwezi kuzungumzia mapinduzi ya viwanda bila kuzungumzia mapinduzi ya kilimo.

ii. Kuweka na kutekeleza mkakati wa kuchochea uwekezaji katika viwanda vyenye kulenga kuzalisha bidhaa zitakazoifanya nchi ijitosheleze kwa mahitaji ya bidhaa muhimu na kukuza mauzo ya bidhaa zilizoongezwa thamani nje ya nchi.

iii. Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuchochea ukuaji wa sekta binafsi, hususan tukilenga kuweka mazingira maalumu ya kukuza na kuimarisha biashara na uwekezaji mdogo na wa kati (small and medium enterprises);

iv. Kulinda na kusimamia matumizi endelevu ya raslimali za taifa, zikiwemo gesi, madini, misitu, bandari, maziwa, n.k. Mwelekeo wa kisera wa Serikali ya CCM ni kutumia raslimali hizi kama msingi wa kujenga uchumi wa viwanda kwa kuweka mkazo katika kuongeza thamani mazao yatokanayo na raslimali za asili za Taifa letu. Serikali itahakikisha kuwa nchi yetu inapunguza na hatimaye kuzuia kabisa kusafirisha kama mali ghafi raslimali zinazovunwa kutoka katika ardhi, misitu na maji ya Tanzania, bali kuweka mazingira ya kisera na kisheria yatakayohakikisha kuwa raslimali hizi zinachakatwa na kuongezwa thamani nchini kabla ya kusafirishwa nje ya nchi.

v. Kwa kuzingatia nafasi ya madini katika kuendelea kukuza ujazo wa mauzo ya bidhaa zetu nje ya nchi, na kwa kuzingatia umuhimu wa madini ya kimkakati (strategic mineral resources-SMR) katika kutimiza azima ya dunia ya kuzalisha nishati safi na salama kwa mazingira, tutaweka mazingira mahususi kwa lengo la kuvutia wawekezaji watakaokuwa tayari kujenga viwanda vya kuongeza thamani ya madini hapa nchini, hususan katika ujenzi wa viwanda vya kuzalisha betri za magari na mitambo.

vi. Kwa kuzingatia kuwa raslimali watu ndio injini ya maendeleo na ndio raslimali kubwa zaidi tuliyo nayo kama Taifa, na kwa kuzingatia idadi kubwa (76%) ya watoto na vijana chini ya umri wa miaka 35 katika nchi

yetu, serikali itaendelea kuwekeza katika kuhakikisha kuwa nchi yetu ina raslimali watu wa kutosha na wenye ubora unaokidhi mahitaji ya dunia ya leo na kesho. Hivyo basi, elimu na mafunzo itaendelea kuwa kipaumbele mama katika mipango ya maendeleo ya Taifa letu.

vii. Kwa kuzingatia nafasi na umuhimu wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji, pamoja na miundombinu ya kidigitali, katika kuchochea maendeleo ya uchumi, Serikali itaendelea kuwekeza katika ujenzi na utunzaji wa miundombinu hii kwa kushirikiana na sekta binafsi.

viii. Kuendelea kuimarisha uzalishaji wa nishati kama nyenzo muhimu katika ujenzi wa uchumi wa viwanda, pamoja na kutekeleza kikamilifu mkakati wa matumizi ya nishati safi ya kupikia.

ix. Kuendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za kutosheleza za jamii, zikiwemo afya, maji na umeme, hususan katika maeneo ya vijijini.

x. Kwa kuzingatia kuwa sehemu kubwa ya wananchi wanaishi vijijini (65%), na katika kuchochea ukuaji wa uchumi jumuishi, Serikali itaweka mkazo maalum katika kuchochea maendeleo vijijini kwa kuchukua hatua tano zifuatazo:

   a. Kuendelea kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu ya barabara na mawasiliano vijijini kwa kuimarisha na kuiwezesha zaidi TARURA;

   b. Katika kuongeza kasi na kiwango cha wananchi wa vijijini kutumia teknolojia ya habari katika shughuli za kiuchumi na kijamii, Serikali itaendelea kutekeleza mradi wa mawasiliano vijijini (mobile network rural coverage project) na kuanzisha na kutekeleza mpango maalum wa kuunganisha vijijini kidigitali (rural broadband programme);

   c. Serikali itapitia upya mfumo wa uuzaji wa mazao ya kilimo, mifugo, na misitu kwa lengo la kurahisisha na kuwezesha mazingira ya kufanya biashara vijijini;

   d. Kuweka mazingira maalum katika kuvutia ujenzi wa viwanda vidogo vijijini kwa lengo la kufanya ongezeko la awali la thamani (primary processing) katika sekta za kimkakati, zikiwemo kilimo, mifugo, uvuvi, na misitu. Serikali itatumia sera za kifedha na kikodi ili kuvutia wawekezaji katika maeneo ya vijijini ili mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na misitu yatoke vijijini yakiwa yameanza

kufanyiwa uchakataji wa awali (semi-processed). Viwanda vya vijijini vitabakisha thamani kubwa kijijini na kutoa nafasi ya ajira kwa vijana na wanawake ambao wengi wao sasa wana elimu ya sekondari. Katika hatua hii, tutahitaji kulipanga upya shirika la viwanda vidogo nchini (SIDO); na

e. Kupitia upya sera za fedha, sheria na kanuni zinazosimamia mikopo kwa lengo la kuzisukuma taasisi za kifedha kuelekeza mikopo katika sekta ya kilimo, ufugaji, uvuvi, na wachimbaji wadogo wa madini vijijini.

35 ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia mpango huu ninaouwasilisha hapa na mipango ambayo waheshimiwa mawaziri wa kisekta waliwasilisha kupitia hotuba za bajeti zao, pamoja na michango ya waheshimiwa wabunge, hakuna shaka kuwa sisi wabunge na watanzania kwa ujumla tunaijua nchi yetu vizuri, tunajua tulipo, na tunajua tunapotaka kwenda na namna ya kufika huko. Hata hivyo, kuwa na mipango mizuri ni jambo moja, na kuitekeleza mipango hiyo kikamilifu ni jambo lingine. Hivyo, katika hatua inayofuata baada ya Bunge kupitisha mipango na bajeti ya Serikali ni muhimu kujipanga katika kusimamia utekelezaji wake kikamilifu.

36 ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imejipanga kuimarisha mfumo wa usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa programu na miradi ambayo Bunge lako tukufu limeipitisha hapa. Mfumo huu umejengwa katika nguzo tatu, ambayo ni: kuainisha vipaumbele bayana na kwa uwazi kwa kila sekta (prioritisation); nidhamu ya utekelezaji (discipline of implementation); na uwajibikaji (accountability). Katika kutekeleza mfumo huu, kuanzia mwaka ujao wa fedha unaonza tarehe 01 Julai 2024, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ameelekeza Serikali kutekeleza hatua sita (6) zifuatazo:

i. Kila sekta inayotekeleza programu na miradi ya maendeleo itaweka bayana malengo na matokeo ya utekelezaji yanayopimika (Key Performance Indicators-KPI), pamoja na kazi mbalimbali zitakazofanyika kufikia malengo hayo.

ii. Taarifa ya utekelezaji itawasilishwa kwa Waziri wa sekta husika kwa kila wiki. Waziri husika atawasilisha taarifa ya utekelezaji kila mwezi kwa Tume ya Mipango.

iii. Tume ya Mipango itatoa Taarifa ya utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo kwa umma kila mwaka kupitia tukio la wazi

iv. Kwa kuzingatia Kifungu cha 7 cha Sheria ya Tume ya Mipango, 2023, Tume itakuwa na mamlaka ya kuitisha vikao vya viongozi wa juu wanaosimamia utekelezaji wa programu na miradi kwa lengo la kuratibu uchambuzi wa changamoto za utekelezaji na kusukuma utekelezaji wa suluhu zilizokubalika ili kuondoa vikwazo vya utekelezaji, kuboresha uratibu na kupata taarifa kwa wakati mwafaka.

# E. Hitimisho

37 ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25 niliouwasilisha ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26, ambao umetokana na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020.

38 ***Mheshimiwa Spika,*** msingi wa sera za CCM ni maendeleo ya watu. Tunapowekeza katika ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, anga, n.k. tunafanya hivyo kama nyenzo ya kuleta maendeleo ya watu. Tunapowekeza katika kuongeza idadi ya majengo ya shule kutatafsiriwa tu kama tendo la maendelo ya watu kama hatimaye majengo hayo yanatumika kuongeza ujuzi na elimu kwa watu wetu. Hivyo hivyo, kuongezeka kwa mazao ya chakula na biashara ni tendo tu la maendeleo kama hatimaye watu wetu watapata chakula bora na kwamba mazao ya biashara hatimaye yatauzwa kwa bei nzuri na kuwapatia wakulima fedha zitakazotumika kununulia vitu vitakavyoboresha afya zao na kuwapa furaha zaidi.

39 ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango tuliouwasilisha na mipango yote inayowasilishwa katika Bunge hili ni kwa ajili ya maendeleo ya watu. Na ndiyo maana viashiria vya mafanikio vilivyowekwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano vinalenga kupima maendeleo ya watu. Hivyo, tuendako, upimaji wetu wa mafanikio katika utelekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo utazingatia sana, pamoja na vigezo vingine, viashiria vinavyopima maendeleo ya watu kuliko kupima tu kazi zilizofanyika.

40 ***Mheshimiwa Spika,*** Hayati Benjamin Mkapa, Rais wa tatu wa Tanzania, aliwahi kutuasa "Kuzeeka peke yake ndio inaweza kutokea bila kupanga". Lakini maendeleo ya kweli yatatokana na mipango mizuri na nidhamu ya utekelezaji wa mipango hiyo. Akihutubia katika Mkutano wa Halmashauri Kuu ya CCM, Dodoma, tarehe 25 Agosti 2004, Rais Benjamin William Mkapa, alisisitiza umuhimu wa mipango mizuri kwa kusema: "Kuongoza ni kupanga kwanza. Mipango mizuri huleta maamuzi mazuri kimkakati na kiutendaji".

41 ***Mheshimiwa Spika,*** Chama Cha Mapinduzi ni chama kiongozi, na kuongoza ni kuonyesha njia. Nina imani kuwa Mpango wa Maendeleo niliouwasilisha hapa ni mpango sahihi unaoakisi maono ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan na Ilani ya CCM. Sisi kama Serikali tumejipanga vizuri kutekeleza mpango huu.

42 ***Mheshimiwa Spika,*** ninapohitimisha ninaomba kutumia fursa hii kuwashukuru wadau wote wa maendeleo wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, Madiwani, Washirika wa Maendeleo, Taasisi za Elimu na Tafiti, Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia, Taasisi za Dini na Wananchi wote kwa namna walivyojitoa na kushiriki kikamilifu katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuimarisha uchumi wa Taifa letu. Wadau hao wamekuwa na mchango mkubwa katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo. Kwa msingi huo, niwaombe kuendelea kushirikiana na Serikali yetu inayoongozwa na Jemedari Shupavu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

43 ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kumshukuru Mke wangu na rafiki yangu wa karibu zaidi, Prosista Laswai, pamoja na watoto wetu, Ntandu, Calvin na Nsumbu, kwa upendo wao na ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kifamilia na kiofisi kama Mbunge wa Jimbo la Ubungo na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Ninawapenda sana kama wao wanavyonipenda!

44 ***Mheshimiwa Spika,*** kwa umuhimu mkubwa, niwashukuru wananchi wenzangu wa Jimbo la Ubungo kwa ushirikiano wanaonipatia tunapoendelea kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi katika kujiletea maendeleo ikichagizwa na kauli mbiu yetu: Ubungo Yetu, Fahari Yetu!

45 ***Mheshimiwa Spika,*** Hotuba hii na vitabu vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25 na Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2023 vinapatikana katika tovuti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji (**www.planninginvestment.go.tz ).**

46 ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo ninaomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili, Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25.

47 ***Mheshimiwa Spika,*** Ninaomba Kutoa Hoja!

**Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji**
**Mji wa Serikali - Mtumba 1 Barabara ya Ardhi,**
**S.L.P. 104, 40403 DODOMA.**

**www.planninginvestment.go.tz**

**@ofisiya_Rais_Mu** **@ormipango_uwekezaji** **@ORmipangoUwekezajiTV**